Journal of Kiswahili and Other African Languages
Vol. 4 No. 2 (2026): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/3kg86r52
Usawiri wa Mwanamke wa Kimfumojike Katika Tamthilia za Kiswahili: Uchambuzi wa Mama Mtakatifu (1982) na Kivuli Kinaishi (1990)

Usawiri wa Mwanamke wa Kimfumojike Katika Tamthilia za Kiswahili: Uchambuzi wa *Mama Mtakatifu* (1982) na *Kivuli Kinaishi* (1990)

Felix Kwame Sosoo
University of Ghana

Article History
Received: 02.04.2026
Revised: 20.09.2026
Accepted: 28.09.2026
Published: 03.10.2026

Keywords
Mama mtakatifu
Mfumojike
Ufeministi wa Kiafrika
Usawiri wa mwanamke

How to cite:
Sosoo, F. K. (2026). Usawiri wa Mwanamke wa Kimfumojike Katika Tamthilia za Kiswahili: Uchambuzi wa *Mama Mtakatifu* (1982) na *Kivuli Kinaishi* (1990). *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 4*(2), 1-12.

Copyright © 2026

Ikisiri
Makala hii inachunguza usawiri wa mwanamke wa kimfumojike katika tamthilia za Kiswahili kwa kurejelea *Mama Mtakatifu* (1982) ya Felix Osodo na *Kivuli Kinaishi* (1990) ya Said Ahmed Mohamed. Lengo ni kubainisha namna mwanamke anavyosawiriwa katika nafasi za mamlaka, uongozi, na uwajibikaji wa kijamii. Utafiti umetumia mkabala wa kitaamuli, ambapo data zimepatikana kupitia usomaji wa kina wa tamthilia teule na kuchanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi wa kimaudhui. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imetumika kuongoza ufafanuzi wa nafasi ya mwanamke kwa kuzingatia mazingira ya Afrika ya kijamii, kiutamaduni, na kihistoria. Matokeo yanaonesha kuwa tamthilia hizi zinamsawiri mwanamke kama kiongozi wa ngazi ya juu, mwenye mamlaka ya kufanya maamuzi, msimamizi wa shughuli za kiutamaduni na ustawi wa jamii, mshiriki katika uongozi wa baraza la wazee, mrithi wa madaraka, na mhusika mwenye hekima, nguvu za kiroho na uwezo wa uganga. Usawiri huu unaonesha kuwa fasihi ya Kiswahili inaweza kuibua mifumo ya kijamii inayompa mwanamke mamlaka na nafasi kubwa katika uendeshaji wa jamii. Hivyo, makala inachangia mjadala kuhusu uwakilishi wa mwanamke kwa kuonesha taswira inayotofautiana na ile ya mwanamke tegemezi katika mifumo ya kimfumodume, na kusisitiza umuhimu wa kuchunguza mazingira ya kijamii yanayounda mamlaka ya wanawake.

Utangulizi

Mwanamke amekuwa sehemu muhimu ya uwakilishi katika fasihi ya Afrika, ambapo waandishi humjenga katika nafasi mbalimbali zinazohusiana na familia, uzalishaji mali, utamaduni, uongozi, na mahusiano ya kijamii. Katika baadhi ya tafiti, uwakilishi huo umehusishwa na mifumo ya kijamii inayomweka mwanamke katika nafasi tegemezi au chini ya mamlaka ya wanaume (Amadiume, 1987; Oyěwùmí, 1997). Hata hivyo, fasihi ya Afrika pia ina matini zinazomjenga mwanamke akiwa na mamlaka, akifanya maamuzi na kushiriki katika uendeshaji wa jamii. Kwa hiyo, uwakilishi wa mwanamke haupaswi kueleweka kwa kumtazama pekee kama mhusika aliye katika nafasi ya utegemezi.

Katika fasihi ya Kiswahili, suala la taswira na nafasi ya mwanamke limejadiliwa na watafiti mbalimbali. Balisidya (1982) alichunguza taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi ya Tanzania,

huku Lihamba (1979) akijadili uwakilishi wa mwanamke katika sanaa za maonesho na fasihi ya Tanzania. Mbughuni (1982), kwa upande wake, alijadili taswira ya mwanamke katika nathari ya Kiswahili. Tafiti hizi zinaonesha kuwa mwanamke amekuwa mhusika muhimu katika kujenga na kuibua masuala ya kijamii na kiutamaduni katika fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, mjadala huu haujaelekeza kwa kiwango cha kutosha katika namna mwanamke anavyosawiriwa akiwa na mamlaka ya uongozi, urithi na kufanya maamuzi katika mazingira ya kimfumojike.

Dhana ya *kimfumojike* katika makala hii inarejelea usawiri wa mazingira ya kijamii ambamo mwanamke anapewa au anashikilia nafasi kuu za mamlaka, uongozi na kufanya maamuzi. Dhana hii haitumiki kumaanisha tu ubadilishaji wa nafasi kati ya wanaume na wanawake, wala haimaanishi kwamba kila jamii yenye urithi wa upande wa mama ni ya kimfumojike. Badala yake, inazingatia namna matini inavyomjenga mwanamke kama mtu mwenye uwezo wa kumiliki, kutumia na kuendeleza mamlaka katika mazingira mahsusi ya kijamii na kiutamaduni. Mtazamo huu unaendana na misingi ya Ufeministi wa Kiafrika inayosisitiza kuchunguza uzoefu na nafasi ya mwanamke kwa kuzingatia historia, utamaduni, na mahusiano ya kijamii ya mazingira yake (Amadiume, 1987; Nnaemeka, 2004).

Katika muktadha huo, *Mama Mtakatifu* (1982) ya Felix Osodo na *Kivuli Kinaishi* (1990) ya Said Ahmed Mohamed ni matini zinazofaa kuchunguza namna mwanamke anavyosawiriwa akiwa katika nafasi ya mamlaka. Katika *Mama Mtakatifu*, Mama Mtakatifu na Linda Zawadi wanahusishwa na uongozi, urithi wa madaraka, kufanya maamuzi, na masuala yanayogusa maisha ya wananchi. Katika *Kivuli Kinaishi*, Bi. Kirembwe anajitambulisha kama mrithi wa jadi wa Giningi na mwenye haki ya kushikilia kiti cha utawala. Matini hizi, kwa hiyo, zinatoa fursa ya kuchunguza si tu uwepo wa mwanamke katika nafasi ya mamlaka, bali pia namna mamlaka hayo yanavyojengwa, kuhalalishwa na kutumiwa.

Ingawa tafiti zilizotangulia zimechangia mjadala kuhusu taswira na nafasi ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili, bado kuna haja ya kuchunguza kwa umahsusi usawiri wa mwanamke mwenye mamlaka katika mazingira ya kimfumojike yanayojitokeza katika tamthilia. Pengo hili, ndilo linalolengwa na makala hii kwa kuchanganua namna matendo, kauli, maamuzi, urithi, mahusiano na nafasi za kijamii za wahusika wanawake zinavyotumika kujenga usawiri wao wa kimfumojike. Kwa msingi huo, lengo kuu la makala hii ni kuchunguza usawiri wa mwanamke wa kimfumojike katika *Mama Mtakatifu* (1982) na *Kivuli Kinaishi* (1990). Ili kufikia lengo hilo, makala inalenga kubainisha namna wahusika wanawake wanavyosawiriwa katika nafasi za uongozi, mamlaka na kufanya maamuzi; kuchanganua namna urithi, uzoefu, mahusiano ya kijamii na ushiriki katika shughuli za jamii vinavyojenga usawiri wa mwanamke wa kimfumojike; na kutathmini namna matumizi ya mamlaka ya wahusika wanawake yanavyoathiri mahusiano na ustawi wa jamii katika tamthilia teule. Uchambuzi wa malengo haya unaongozwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, ambayo inasaidia kutafsiri mamlaka ya wanawake kwa kuzingatia mazingira ya kijamii, kiutamaduni, na kihistoria.

Msingi wa Kinadharia

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, inayochunguza nafasi na uzoefu wa mwanamke kwa kuzingatia mazingira ya Afrika ya kihistoria, kiutamaduni, kijamii, na kiuchumi. Nadharia hii iliibuka kutokana na haja ya kuendeleza mitazamo ya kifeministi inayozingatia hali halisi ya wanawake wa Afrika, badala ya kutumia kwa jumla dhana zilizoundwa katika mazingira ya Kimagharibi. Steady (1981), Amadiume (1987), na Nnaemeka (2004) ni

miongoni mwa wataalamu waliochangia kuendeleza mjadala huu. Kwa mtazamo huu, mwanamke wa Kiafrika hafafanuliwi pekee kama mhanga wa ukandamizaji wa kijinsia, bali pia kama mshiriki katika uzalishaji, malezi, utamaduni, uongozi, na maendeleo ya jamii.

Nadharia hii inasisitiza kuwa uzoefu wa mwanamke huathiriwa na mwingiliano wa utamaduni, historia, uchumi, na mahusiano ya kijamii. Kwa hiyo, uchambuzi wa nafasi ya mwanamke unapaswa kuzingatia mazingira yanayomzunguka na namna mamlaka yanavyogawanywa katika jamii. Mtazamo huu unafaa kwa makala hii kwa sababu unaruhusu kuchunguza usawiri wa mwanamke katika mazingira ya kimfumojike bila kudhani kwamba mamlaka ya mwanamke ni nakisi au mwigo wa mamlaka ya mwanaume.

Katika uchambuzi wa tamthilia teule, nadharia hii imetumika kuangalia namna wahusika wanawake wanavyopewa mamlaka na kutekeleza majukumu ya kijamii. Vipengele vilivyozingatiwa ni uongozi na mamlaka ya kufanya maamuzi; nafasi katika urithi na uendelezaji wa taasisi za jamii; usimamizi wa shughuli za kiutamaduni na ustawi wa jamii; ushirikiano na baraza la wazee; pamoja na matumizi ya hekima, nguvu za kiroho, na uganga. Vipengele hivi havikuchukuliwa kama orodha ya sifa, bali kama maeneo ya kuchunguza namna mamlaka ya mwanamke inavyojengwa na kuhalalishwa ndani ya matini.

Kwa msingi huo, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imesaidia kufasiri matendo, maamuzi, majukumu na mahusiano ya wahusika wanawake katika *Mama Mtakatifu* (1982) na *Kivuli Kinaishi* (1990). Hivyo, nadharia imewezesha makala kuchunguza si tu uwapo wa mwanamke katika nafasi za mamlaka pekee, bali pia maana ya nafasi hizo katika mfumo wa kijamii unaowasilishwa na tamthilia. Katika makala hii, dhana ya kimfumojike inahusishwa na usawiri wa mamlaka ya mwanamke ndani ya jamii za kifasihi zinazowasilishwa na waandishi. Kwa hiyo, haichukuliwi kuwa sawa moja kwa moja na mfumo wa urithi wa kimama, kwa kuwa urithi wa upande wa mama pekee haujitoshelezi kuthibitisha kwamba mamlaka yote ya kisiasa au kijamii yako mikononi mwa wanawake. Mtazamo huu umewezesha uchambuzi kubaki katika ushahidi wa matini na kuepuka kuhusisha tamthilia na madai ya jumla kuhusu jamii zote za Afrika.

Mbinu za Utafiti

Makala hii, ilitumia mkabala wa kitaamuli kwa kuwa ulilenga kuchanganua na kutafsiri namna usawiri wa mwanamke wa kimfumojike unavyojengwa katika tamthilia teule. Mkabala huu, ulifaa kwa sababu utafiti haukulenga kupima matukio kwa kutumia takwimu, bali kuchunguza maana zinazojengwa kupitia kauli, matendo, maamuzi, mahusiano, na nafasi za wahusika wanawake katika matini. Tamthilia mbili, ambazo ni *Mama Mtakatifu* (1982) ya Felix Osodo na *Kivuli Kinaishi* (1990) ya Said Ahmed Mohamed, ziliteuliwa kimakusudi kwa kuwa zinawasilisha wahusika wanawake katika nafasi zinazohusisha uongozi, mamlaka, urithi, kufanya maamuzi, na ushiriki katika masuala ya kijamii na kiutamaduni. Uteuzi huu, uliwezesha kuchunguza na kulinganisha namna usawiri wa mwanamke wa kimfumojike unavyojengwa katika matini hizi mbili.

Data za msingi zilikusanywa kupitia usomaji wa kina wa tamthilia teule. Katika mchakato huo, vifungu vinavyohusiana na usawiri wa mwanamke wa kimfumojike vilitambuliwa, kuchaguliwa, na kurekodiwa kwa kuzingatia maudhui na muktadha wake katika matini. Data zilihusisha kauli za wahusika, matendo yao, maamuzi wanayofanya, nafasi wanazoshikilia, mahusiano yao na wahusika wengine, pamoja na matukio yanayoonesha chanzo, uhalali na matumizi ya mamlaka yao. Dondoo kutoka katika tamthilia zilitumika kama ushahidi wa msingi katika uchambuzi. Aidha, vitabu na makala za kitaaluma zinazohusiana na Ufeministi wa Kiafrika, usawiri wa mwanamke, na

fasihi ya Kiswahili zilitumika kama vyanzo vya ziada vya kuimarisha mjadala wa kinadharia na kimuktadha.

Data zilizokusanywa zilipangwa kulingana na maeneo yanayohusiana na lengo la utafiti na kuchanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi wa kimaudhui. Uchambuzi ulijikita katika namna wanawake walivyosawiriwa katika nafasi za uongozi na mamlaka, kufanya maamuzi, kushiriki katika shughuli za kijamii na kiutamaduni, uongozi shirikishi, kurithi mamlaka na kutumia uzoefu au maarifa katika uendeshaji wa jamii. Katika kila eneo, dondoo kutoka katika tamthilia zilitumika kama ushahidi wa msingi, zikafafanuliwa kwa kuzingatia muktadha wa tukio na kisha kutafsiriwa kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Kwa hiyo, uchambuzi haukuishia katika kubainisha sifa za wahusika wanawake tu, bali ulilenga kueleza namna matini inavyowajenga kama wahusika wenye mamlaka, chanzo cha mamlaka hayo, namna yanavyohalalishwa na jinsi yanavyotumiwa katika mahusiano yao na jamii. Ulinganisho kati ya tamthilia hizo mbili ulifanywa pale ambapo data zilionesha mfanano au tofauti katika ujenzi wa usawiri huo. Makala imejikita katika tamthilia hizi mbili pekee na, kwa hiyo, matokeo yake hayakusudii kuwakilisha tamthilia zote za Kiswahili wala kutoa hitimisho kuhusu wanawake katika jamii zote za Kiafrika. Badala yake, unalenga kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu namna mwanamke wa kimfumojike anavyosawiriwa katika matini hizi na jinsi mazingira ya kijamii na kiutamaduni yanavyohusiana na ujenzi na matumizi ya mamlaka ya wahusika wanawake.

Matokeo na Majadiliano

Sehemu hii inawasilisha na kujadili matokeo ya uchanganuzi wa *Mama Mtakatifu* (1982) na *Kivuli Kinaishi* (1990), kwa kuzingatia namna mwanamke anavyosawiriwa katika mazingira yenye misingi ya kimfumojike. Uchanganuzi umeongozwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, inayosisitiza kutafsiri nafasi ya mwanamke kwa kuzingatia mazingira ya kijamii, kiutamaduni na kihistoria ya Afrika (Steady, 1981; Amadiume, 1987; Nnaemeka, 2004). Matokeo yanaonesha kuwa wahusika; Mama Mtakatifu, Linda Zawadi, na Bi Kirembwe wamesawiriwa katika nafasi za mamlaka zinazohusisha uongozi, urithi, maamuzi, na usimamizi wa jamii. Hata hivyo, mamlaka hayo hayawasilishwi kuwa mazuri kwa sababu tu yanashikiliwa na wanawake; matumizi yake yanaoneshwa kuwa yanaweza kujenga au kukandamiza. Kwa hiyo, uchanganuzi unaofuata haujikita katika kutaja sifa za wahusika pekee, bali unaunganisha dondoo kutoka katika tamthilia na mazingira ya matukio, kisha kuzifasiri kwa kuzingatia dhana za Ufeministi wa Kiafrika. Kwa mtazamo huu, usawiri wa mwanamke unachunguzwa kama ujenzi wa kifasihi unaoonesha namna mamlaka ya mwanamke yanavyotambuliwa, kuhalalishwa, na kutumiwa katika jamii zinazowasilishwa na waandishi.

Mwanamke kama Kiongozi wa Ngazi ya Juu

Uongozi wa kiwango cha juu ni mojawapo ya namna muhimu ambazo mwanamke anasawiriwa katika tamthilia teule. Badala ya kuwasilishwa kama mhusika anayesubiri maamuzi ya wanaume, mwanamke anajengwa kama mtu mwenye mamlaka ya juu na anayehusika moja kwa moja na uendeshaji wa jamii. Katika *Mama Mtakatifu*, nafasi hii inadhihirika kupitia Mama Mtakatifu na mrithi wake, Linda Zawadi. Dondoo linalohusiana na urithi wa Linda linaeleza:

> "Ewe Linda Zawadi mtoto wa kike wa Mama Mtakatifu, kalia kiti hiki cha enzi utawale wananchi wa nchi hii ya Haki kama vile Mamako alivyotawala" (uk.13).

Kauli hii inamweka Linda katika nafasi ya mtawala na inaunganisha uhalali wa uongozi wake na urithi wa upande wa mama. Hivyo, usawiri huu hauishii katika kumpa mwanamke hadhi ya heshima tu, bali unamjenga kama mhusika mwenye mamlaka ya kuongoza jamii.

Jambo muhimu katika dondoo hili ni matumizi ya maneno "kalia kiti hiki cha enzi" na "utawale wananchi". Maneno hayo yanaonesha kuwa mamlaka anayokabidhiwa Linda ni ya kiuongozi na si ya kifamilia pekee. Aidha, kauli "kama vile Mamako alivyotawala" inaunganisha uongozi wa Linda na ule wa Mama Mtakatifu, hivyo kuonesha mwendelezo wa mamlaka kupitia mstari wa mwanamke. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, usawiri huu ni muhimu kwa sababu unamwonesha mwanamke kama mhusika anayeweza kurithi na kuendeleza mamlaka ya kijamii, badala ya kuwekwa nafasi ya pili katika uongozi kwa misingi ya jinsia. Hata hivyo, dondoo hili linapaswa kutafsiriwa ndani ya ulimwengu wa tamthilia na si kama ushahidi wa jumla kuhusu jamii za Kiafrika.

Katika *Kivuli Kinaishi*, usawiri wa mwanamke kama mtawala unaonekana kupitia Bi Kirembwe, kiongozi wa Giningi. Serikali ya Giningi inaongozwa na Bi Kirembwe akisaidiwa na wazee. Zaidi ya hayo, Bi Kirembwe mwenyewe anajitambulisha kwa kauli:

"Mimi ndiye mrithi wa jadi wa Giningi. Ndiye mchawi mkuu ndiye mwenye kustahiki kukalia kiti hiki… daima dawamu" (uk. 71). Kauli hii ni ushahidi wa moja kwa moja wa namna anavyojenga uhalali wa mamlaka yake. Anajitaja kama "mrithi wa jadi" na "mwenye kustahiki kukalia kiti", hivyo kuunganisha uongozi, urithi na mamlaka ya kijamii katika nafsi yake. Dondoo hilo pia limetumiwa katika utafiti wa taswira ya *Kivuli Kinaishi* kuonesha madai ya Bi Kirembwe kuhusu uhalali wake wa kutawala.

Hata hivyo, usawiri wa Bi Kirembwe unatofautiana na ule wa Linda kwa sababu mamlaka yake yanaoneshwa pia kupitia udhibiti na ukandamizaji. Maelezo ya mchapishaji wa *Kivuli Kinaishi* yanaonesha Giningi kama jamii yenye utawala wa amri moja chini ya Bi Kirembwe, akisaidiwa na wazee, huku ukatili ukiwa sehemu muhimu ya utawala huo. Kwa hiyo, mwandishi haishii katika kuthibitisha kwamba mwanamke anaweza kuwa mtawala; anaonesha pia kwamba mamlaka yanaweza kutumiwa vibaya bila kujali jinsia ya mtawala. Hili linaifanya dhana ya usawiri kuwa pana zaidi kuliko kutaja "uongozi wa mwanamke" kama sifa.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, wahusika hawa wanatoa taswira ya mwanamke mwenye uwezo wa kushika mamlaka katika mazingira yanayohalalisha uongozi wake. Hata hivyo, tamthilia zote mbili zinaonesha tofauti kati ya kuwa na mamlaka na namna mamlaka hayo yanavyotumiwa. *Mama Mtakatifu* inasisitiza mwendelezo wa uongozi kupitia urithi wa Linda, wakati *Kivuli Kinaishi* inasisitiza zaidi uhalali unaodaiwa na Bi Kirembwe pamoja na athari za utawala wake. Kwa hiyo, usawiri wa mwanamke kama kiongozi wa ngazi ya juu katika tamthilia hizi unapanua uelewa wa nafasi ya mwanamke kwa kumweka katikati ya mamlaka ya kisiasa na kijamii, huku ukionesha kwa wakati mmoja uwezekano wa mamlaka hayo kuwa na matokeo tofauti.

Mwanamke kama Mtu Mwenye Mamlaka ya Kufanya Maamuzi

Uongozi wa juu unaojitokeza katika sehemu iliyotangulia unaambatana na mamlaka ya kufanya maamuzi. Katika tamthilia teule, mwanamke hasawiriwi tu kama mwenye cheo cha uongozi, bali kama mhusika anayefanya maamuzi yanayoathiri sheria, mwenendo na maisha ya jamii. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, mamlaka haya yanapaswa kuchunguzwa ndani ya mazingira

ya kijamii na kiutamaduni yanayompa mwanamke uhalali wa kuyatumia (Steady, 1981; Nnaemeka, 2004).

Katika *Mama Mtakatifu*, mamlaka ya kufanya maamuzi yanaonekana kupitia sheria zilizowekwa na Mama Mtakatifu katika nchi ya Haki. Miongoni mwa mambo aliyodhibiti ni matumizi ya pombe ya chang'aa, chakula na mwenendo wa wananchi. Nguvu ya maamuzi hayo inaelezwa wazi katika kauli: "zote zilifuatwa na kila mwananchi wa Haki na hakuna aliyeweza kuthubutu kuhoji wala kupinga" (uk. 11). Dondoo hili linamsawiri Mama Mtakatifu kama chanzo cha kanuni zinazotekelezwa na jamii bila kupingwa. Hata hivyo, baadhi ya maamuzi yake yanaoneshwa pia kuwa na upande wa udhibiti, jambo linaloonesha kwamba kuwa mwanamke mwenye mamlaka hakumaanishi kwamba matumizi ya mamlaka hayo ni ya haki kila wakati.

Mamlaka hayo yanaonekana pia katika hatua za kulinda utawala wake. Mama Mtakatifu anapiga marufuku mikutano ya usiku iliyofanywa na wanaume waliokuwa wakipanga kuuangusha utawala wake (uk. 7). Hatua hii inamsawiri kama mtawala anayefuatilia vitendo vinavyotishia mamlaka yake na kuchukua hatua dhidi yake. Kwa hiyo, usawiri wa mwanamke katika sehemu hii unajengwa kupitia uwezo wake wa kufanya maamuzi na kuyatekeleza, si kwa nafasi yake ya cheo pekee.

Baada ya Mama Mtakatifu kuondoka madarakani, Linda Zawadi anaendeleza mamlaka ya uongozi huku akitathmini upya baadhi ya kanuni za mtangulizi wake. Katika suala la chang'aa, Linda anaweka msimamo unaohusisha katazo hilo na afya ya wananchi. Msimamo wake unaonekana katika kauli: "Linda: ... pombe chang'aa ni kwa binadamu na hata kwa wanyama wa porini pamoja na majitu. Kwa hivyo napiga marufuku pombe ya chang'aa katika nchi hii ya Haki..." (uk. 11). Dondoo hili linaonesha kwamba mwanamke anasawiriwa kama mtawala mwenye uwezo wa kuweka kanuni kwa kuzingatia hali ya jamii.

Katika *Kivuli Kinaishi*, Bi Kirembwe naye anasawiriwa akiwa na mamlaka ya kuamua na kuhalalisha maamuzi yake kupitia urithi wa jadi. Anasema: "Mimi ndiye mrithi wa jadi wa Giningi. Ndiye mchawi mkuu. Ndiye mwenye kustahiki kukalia kiti hiki ... daima dawamu. ... Huu ni urithi wa jadi" (uk. 70–71). Kauli hii inaunganisha mamlaka yake na urithi, hadhi na utaratibu wa jamii ya Giningi. Aidha, anapokabiliwa na wazee, anasema: "Si mimi nitakayetoa uamuzi, maana nyinyi ni wazee wenzangu..." (uk. 74–75), jambo linaloonesha kuwa maamuzi katika jamii hiyo yanafungamana na mahusiano ya mamlaka na taasisi za wazee.

Kwa hiyo, tamthilia hizi zinamsawiri mwanamke kama mtendaji mwenye uwezo wa kufanya maamuzi yenye athari kwa jamii. Mama Mtakatifu anaweka kanuni na kulinda utawala wake, Linda Zawadi anaendeleza na kutathmini baadhi ya maamuzi hayo, ilhali Bi Kirembwe anahusisha mamlaka yake na urithi wa jadi. Usawiri huu unaonesha kwamba mamlaka ya mwanamke yanajengwa kupitia matendo na maamuzi yake ndani ya mazingira maalumu ya kijamii na kiutamaduni.

Mwanamke katika Uongozi wa Shughuli za Kiutamaduni

Katika tamthilia teule, usawiri wa mwanamke katika shughuli za kiutamaduni haujengwi kwa kumtaja tu kama msimamizi wa mila na sherehe, bali kupitia namna anavyowekwa katika nafasi ya kuongoza na kuelekeza shughuli zinazohusiana na utambulisho na mshikamano wa jamii. Kwa hiyo, kinachochunguzwa hapa ni namna mamlaka ya mwanamke yanavyojitokeza anapohusika katika shughuli za kiutamaduni. Mtazamo huu unaendana na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika

inayosisitiza kuchunguza nafasi ya mwanamke ndani ya mazingira yake ya kijamii na kiutamaduni (Steady, 1981; Nnaemeka, 2004).

Katika *Mama Mtakatifu*, usawiri huu unaonekana kupitia nafasi ya Mama Mtakatifu katika uendeshaji wa sherehe za mapato katika taifa la Haki. Umuhimu wa shughuli hii katika usawiri wa mwanamke unaonekana pia baada ya Mama Mtakatifu kuondoka madarakani. Linda Zawadi, anayechukua nafasi yake, haachi shughuli hiyo, bali anaendeleza maandalizi yake. Mwandishi anaeleza kwamba Linda "aliendelea na maandalizi ya sherehe za mapato" (uk. 19). Matumizi ya kitenzi "aliendelea" yanaonesha mwendelezo wa jukumu la kiuongozi kutoka kwa Mama Mtakatifu kwenda kwa Linda Zawadi. Hivyo, Linda hasawiriwi kama mrithi wa kiti cha enzi pekee, bali pia kama kiongozi anayechukua wajibu wa kuendeleza shughuli iliyokuwa sehemu ya utaratibu wa jamii.

Usawiri huu unaonesha kwamba mamlaka ya mwanamke yanaweza kuhusisha kwa pamoja uongozi wa kisiasa na mwendelezo wa taasisi za kitamaduni. Linda anaporithi mamlaka, anakuwa pia mhusika anayehakikisha kwamba shughuli muhimu kwa jamii zinaendelea. Hali hii inaendana na mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika unaochunguza nafasi ya mwanamke katika mifumo ya kijamii na kitamaduni badala ya kumtenga na taasisi hizo (Steady, 1981; Nnaemeka, 2004). Kwa hiyo, sherehe za mapato zinakuwa sehemu ya kuonesha kwamba uongozi wa mwanamke katika *Mama Mtakatifu* unahusisha pia kulinda mwendelezo wa taratibu za jamii.

Usawiri huo unaonekana pia katika mazingira ya tishio la majitu kutoka Afromlo. Linda anaendelea na maandalizi ya sherehe licha ya hali hiyo, na katika mkusanyiko wa sherehe anashirikiana na wanawake wengine wa Haki katika kukabiliana na tishio hilo. Hivyo, shughuli ya kitamaduni inakuwa mazingira ambamo uongozi na ulinzi wa jamii vinaingiliana. Jambo hili linaifanya nafasi ya Linda katika shughuli za utamaduni kuwa sehemu ya ujenzi wa mamlaka yake ya kiuongozi. Hata hivyo, data haimaanishi kwamba shughuli za kiutamaduni zinahusishwa na wanawake pekee. Kinachoonekana ni kwamba Linda anapewa nafasi ya kuongoza kwa sababu ya nafasi yake katika mfumo wa utawala. Kwa hiyo, usawiri wake unatokana na namna mwanamke anavyowekwa ndani ya taasisi za jamii na kupewa uwezo wa kuzisimamia.

Katika *Kivuli Kinaishi*, usawiri wa mwanamke katika uongozi wa shughuli za kiutamaduni unaonekana kupitia Bi Kirembwe na miviga ya Giningi. Tofauti na *Mama Mtakatifu*, shughuli ya kitamaduni hapa inaoneshwa kupitia tendo la kuwaingiza wari katika mfumo wa Giningi. Bi Kirembwe anatoa maelekezo kwa Mtolewa: "Inama… piga goti tukurambishe unga wa ndere ili tukugeuze… tukurekebishe pepo wako kichwani alingane na pepo wa Giningi" (uk. 52). Dondoo hili linaonesha moja kwa moja kwamba Bi Kirembwe si mtazamaji wa miviga hiyo, bali anatoa maagizo na kushiriki katika utekelezaji wake. Vitenzi "inama", "piga goti", "tukurambishe" na "tukurekebishe" vinaonesha nafasi yake ya kuongoza na kuelekeza tendo hilo.

Uongozi wake unaonekana zaidi anapomwelekeza Mtolewa kufungua kinywa ili aongezewe unga wa ndere. Mwandishi anaandika: "Fungua tena kinywa. (Mtolewa anafungua tena kinywa) Nakuongezea tena unga wa ndere nikuweze" (uk. 53). Data hii inaonesha kwamba Bi Kirembwe ana mamlaka ya kuamua namna miviga inavyotekelezwa na namna mshiriki anavyopaswa kuitikia. Kwa hiyo, usawiri wake unatokana si tu na nafasi yake ya kuwa mtawala, bali pia na matendo yanayoonesha mamlaka yake ndani ya shughuli ya kitamaduni.

Maana ya shughuli hiyo inadhihirika zaidi katika kauli yake baada ya mchakato huo: "Ha…ha…haaaaaaaa! Nimeshinda…ngoma…" (uk. 54). Kauli hii inaonesha kwamba Bi Kirembwe anautazama mchakato huo kama ushindi unaohusiana na utekelezaji wa matakwa yake. Kwa hiyo, miviga haibaki kuwa shughuli ya kitamaduni isiyohusiana na mamlaka; inakuwa sehemu ya mfumo ambao Bi Kirembwe anautumia kuendeleza utawala wake. Hivyo, mwandishi anaonesha uhusiano kati ya utamaduni, utambulisho na mamlaka.

Tofauti kati ya Linda Zawadi na Bi Kirembwe ni muhimu katika kuelewa usawiri wa mwanamke wa kimfumojike. Linda anasawiriwa akihusisha shughuli ya kitamaduni na mwendelezo wa maisha na ulinzi wa jamii, wakati Bi Kirembwe anasawiriwa akitumia miviga kama sehemu ya kuendeleza mfumo wa Giningi na mamlaka yake. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, tofauti hii inaonesha umuhimu wa kuchunguza mamlaka ya mwanamke ndani ya mazingira yake ya kitamaduni na kijamii (Nnaemeka, 2004). Kwa hiyo, tamthilia hizi hazimjengi mwanamke kama msimamizi wa utamaduni kwa maana ya jumla, bali zinaonesha namna anavyotumia nafasi hiyo ndani ya mifumo ya mamlaka. Usawiri wa mwanamke katika shughuli za kiutamaduni, hivyo, unajengwa kupitia matendo yake, nafasi yake katika taasisi za jamii na matokeo ya matumizi ya mamlaka hayo.

Mwanamke katika Uongozi Shirikishi wa Baraza la Wazee

Katika *Mama Mtakatifu* na *Kivuli Kinaishi*, usawiri wa mwanamke katika nafasi ya uongozi haujengwi kwa kumtenga na taasisi nyingine za kijamii. Waandishi wanamweka mwanamke katika mahusiano na wazee, ambao ni sehemu ya mifumo ya uongozi na utawala wa jamii. Hata hivyo, mahusiano hayo yanatofautiana. Katika *Mama Mtakatifu*, uhusiano wa mwanamke kiongozi na wazee unaonekana kupitia mgawanyo wa majukumu ya kiutawala, ilhali katika *Kivuli Kinaishi* unaonekana kupitia mvutano kati ya mamlaka ya Bi Kirembwe na mawazo ya wazee. Kwa hiyo, hoja hapa si kumtaja mwanamke kuwa "mshirikishaji," bali kuchunguza namna anavyosawiriwa ndani ya mfumo wa mahusiano ya mamlaka unaohusisha baraza la wazee.

Katika *Mama Mtakatifu*, usawiri huu unaonekana katika namna baraza la wazee linavyohusika na mwendelezo wa uongozi wa nchi ya Haki. Baada ya kifo cha Mama Mtakatifu kutangazwa, wazee wanahusika katika kuhakikisha urithi wa mamlaka unafuata utaratibu wa jamii. Kizee wa Sheria anauliza: "NI NANI ATAKALIA KITI CHA ENZI?... mimi naonelea ya kuwa katiba ifuatwe." Vizee vinajibu: "Lazima ifuatwe!" Kisha Kizee wa Sheria anasema: "Kufuatana na katiba, Linda Zawadi ndiye Mama Mtakatifu sasa..." (uk. 12). Dondoo hili linaonesha kuwa uongozi wa mwanamke unatambuliwa na taasisi ya wazee kupitia katiba ya jamii. Kwa hiyo, mamlaka ya Mama Mtakatifu na mrithi wake hayawasilishwi kama mamlaka yaliyotengwa na taasisi za kijamii; baraza la wazee linashiriki katika kuhakikisha mwendelezo wa utawala.

Ushiriki wa wazee unaonekana pia wakati Linda Zawadi anapoondoka kwenda Unyankole kutafuta chakula kwa ajili ya wananchi. Katika kipindi hicho, baadhi ya majukumu ya uongozi yanaendelea kusimamiwa na viongozi waliowekwa katika maeneo maalumu. Ngiriama anaeleza: "Nikienda safarini, Wanangiriama wa Sheria na Uhalifu, Njaa na Chakula, na Vita ndio watakaobaki hapa kuwalinda. Yeyote atakayethubutu kuleta nyokonyoko atapelekwa korokoroni" (uk. 34). Ingawa kauli hii inamhusu Ngiriama, inatoa data ya moja kwa moja kuhusu mfumo wa ugawaji wa majukumu katika utawala wa nchi ya Haki. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, jambo hili ni muhimu kwa sababu mamlaka ya mwanamke yanaonekana ndani ya mtandao wa mahusiano na

taasisi nyingine za jamii, badala ya kuwasilishwa kama ushindani wa moja kwa moja kati ya mwanamke na wanaume (Steady, 1981; Nnaemeka, 2004).

Katika *Kivuli Kinaishi*, usawiri wa uhusiano huu unatofautiana. Bi Kirembwe ni mtawala mkuu wa Giningi, lakini wazee hawawasilishwi kama watekelezaji wa maagizo yake pekee. Badala yake, matini inaonesha kuwa wana mitazamo yao kuhusu namna jamii inavyopaswa kuendeshwa. Wazee watatu wanasema: "Tulidhani tutaweza kutoa mchango wetu; tulijisemea tu, tena ndani ya nyoyo zetu kwamba sisi pia tulikuwa na sehemu ya kutaka kuiona Giningi ya namna tofauti kama tunavyofanya" (uk. 74). Kauli "kutoa mchango wetu" inaonesha kwamba wazee walijiona kuwa na nafasi ya kutoa maoni kuhusu uongozi, huku "kuiona Giningi ya namna tofauti" ikifichua uwepo wa mtazamo mbadala kuhusu utawala. Hivyo, mwandishi hawasawiri wazee kama kundi lisilo na sauti, bali kama washiriki wenye fikra kuhusu mustakabali wa jamii.

Hata hivyo, ushiriki huo unawekewa mipaka na mamlaka ya Bi Kirembwe. Matini inaonesha kuwa maoni yanayotofautiana na matakwa ya mtawala yanaweza kuleta madhara kwa wenye kuyatoa. Hali hii inafichua mvutano kati ya uongozi wa mwanamke na taasisi ya wazee. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, mvutano huo ni muhimu kwa sababu nadharia hii huchunguza mamlaka ya mwanamke ndani ya mazingira yake ya kijamii, badala ya kudhani kwamba uwepo wa mwanamke katika nafasi ya juu unatosha kuleta usawa (Amadiume, 1987; Nnaemeka, 2004). Kwa hiyo, Bi Kirembwe anasawiriwa kama kiongozi ambaye mamlaka yake yanaweza kuingia katika mgongano na mitazamo ya taasisi nyingine za jamii.

Kwa ujumla, tofauti kati ya tamthilia hizi mbili inaonesha mitindo miwili ya usawiri wa mwanamke katika uongozi shirikishi. *Mama Mtakatifu* inamsawiri mwanamke kiongozi akiwa ndani ya mfumo ambao baraza la wazee linatambua na kusaidia mwendelezo wa mamlaka, huku *Kivuli Kinaishi* ikimwonesha Bi Kirembwe katika uhusiano wenye mvutano na wazee wenye mitazamo tofauti. Hivyo, usawiri wa mwanamke wa kimfumojike hapa hauishii katika kumweka mwanamke katika nafasi ya juu; unafichua pia namna mamlaka yake yanavyohusiana na taasisi nyingine, namna maoni ya wengine yanavyopokelewa, na mipaka inayowekwa katika ushiriki wa kijamii.

Mwanamke katika Ustawi wa Jamii

Katika *Mama Mtakatifu* na *Kivuli Kinaishi*, usawiri wa mwanamke katika uongozi unaonekana pia kupitia namna mamlaka yake yanavyohusishwa na maisha na ustawi wa wananchi. Ustawi unaonekana kupitia maamuzi kuhusu chakula, vinywaji, afya ya watoto na namna mamlaka inavyoathiri maisha ya wanajamii. Mtazamo huu unaendana na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inayochunguza nafasi ya mwanamke katika mazingira yake ya kijamii na namna anavyoshiriki katika masuala yanayohusu maisha ya jamii (Amadiume, 1987; Nnaemeka, 2004).

Katika *Mama Mtakatifu*, uhusiano kati ya uongozi wa mwanamke na ustawi unaonekana kupitia kanuni zinazohusu maisha ya wananchi wa Haki. Mama Mtakatifu anaweka sheria zinazodhibiti mwenendo wa jamii, na matini inaeleza: "zote zilifuatwa na kila mwananchi wa Haki na hakuna aliyeweza kuthubutu kuhoji wala kupinga" (uk. 11). Kauli yake kuhusu pombe ya chang'aa inaonesha pia maudhui ya afya katika maamuzi yake: "Mama: ... pombe chang'aa ni kwa binadamu na hata kwa wanyama wa porini pamoja na majitu. Kwa hivyo napiga marufuku pombe ya chang'aa katika nchi hii ya Haki..." (uk. 11). Hivyo, mwandishi anamjenga mwanamke mtawala akiwa na uwezo wa kuingilia moja kwa moja suala linalogusa maisha ya kila siku ya jamii.

Usawiri wa mamlaka hayo unapata mwelekeo mwingine kupitia Linda Zawadi. Badala ya kuhusishwa tu na utekelezaji wa sheria, Linda anasawiriwa akichukua maamuzi yanayolenga afya na lishe ya wananchi. Anasema: "Zamani idadi ya watoto ilikuwa ndogo lakini siku hizi imepungua zaidi... wanaume watoe suruali... watoto ... hawana afya njema... kila mama ampe kila mtoto mayai matatu asubuhi" (uk. 15). Dondoo hili linaunganisha uongozi wa Linda na hali ya afya na lishe ya watoto. Kauli yake inaonesha kwamba anatazama ustawi wa jamii kupitia mahitaji ya msingi ya lishe na afya. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, hatua hiyo inamwonesha mwanamke kiongozi akihusika katika mahitaji halisi ya jamii (Amadiume, 1987; Steady, 1981).

Linda pia anazungumzia hali ya wanawake moja kwa moja: "siku hizi wanawake wamekonda... Jambo hili latokana na kutokula kuku... Kwa hiyo ninyi wanawake kuleni kuku!" (uk. 14). Dondoo hili linaonesha kuwa ustawi unahusisha pia hali ya mwili na lishe ya wanawake. Linda, hivyo, anasawiriwa akizingatia mahitaji ya kundi hili. Usawiri huu unaendana na msisitizo wa Ufeministi wa Kiafrika kwamba masuala ya wanawake yanapaswa kueleweka ndani ya mahitaji halisi ya jamii na mazingira yao ya kijamii (Nnaemeka, 2004).

Katika *Kivuli Kinaishi*, usawiri wa mwanamke katika eneo la ustawi unatofautiana. Bi Kirembwe ana mamlaka makubwa juu ya maisha ya Wanaginingi, lakini matini haijengi uongozi wake hasa kupitia sera za afya au lishe. Badala yake, inaonesha namna mamlaka yake yanavyoingia katika maisha ya watu binafsi. Mfano wa moja kwa moja ni tukio la unga wa ndere, ambapo anamwelekeza Mtolewa: "Inama… piga goti tukurambishe unga wa ndere ili tukugeuze… tukurekebishe pepo wako kichwani alingane na pepo wa Giningi" (uk. 52). Kauli hii inaonesha kuwa Bi Kirembwe ana mamlaka ya kuamua namna mtu anavyopaswa "kurekebishwa" ili aendane na utaratibu wa Giningi. Kwa hiyo, hali ya mtu binafsi inakuwa sehemu ya matumizi ya mamlaka ya mtawala.

Aidha, Bi Kirembwe anajieleza kwa kusema: "Mimi ndiyo nguzo inayobeba maslahi yenu. Ikitenguka nguzo hiyo na nyinyi mmeanguka. Mimi ndiyo mhimili wa umoja wenu... Mimi ndiye mtetezi wa maslahi ya Giningi" (uk. 72). Kauli hii inajenga taswira ya kiongozi anayejiona kama msingi wa maslahi na umoja wa jamii. Ikisomwa pamoja na dondoo la unga wa ndere, kauli hii inaonesha mvutano kati ya madai ya kulinda maslahi ya jamii na matumizi ya mamlaka juu ya mtu binafsi. Hivyo, mwandishi hamjengi Bi Kirembwe kama mlezi wa jamii kwa namna isiyo na utata, bali anaonesha ugumu wa uhusiano kati ya mamlaka, maslahi ya jamii na uhuru wa mtu binafsi.

Kwa ujumla, tamthilia hizi mbili zinatoa mitazamo tofauti kuhusu usawiri wa mwanamke katika ustawi wa jamii. *Mama Mtakatifu* anaoneshwa akitumia mamlaka katika kudhibiti mambo yanayogusa maisha ya wananchi, huku Linda Zawadi akihusishwa moja kwa moja na masuala ya lishe na afya ya watoto na wanawake. Bi Kirembwe, kwa upande mwingine, anasawiriwa kupitia matumizi ya mamlaka yanayoathiri maisha na hali ya mtu binafsi. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, tofauti hizi zinaonesha kuwa nafasi ya mwanamke katika jamii haiwezi kueleweka kwa kuangalia tu uwepo wake katika uongozi; inahitaji kuchunguza namna mamlaka yake yanavyotumika na athari zake kwa maisha ya jamii (Steady, 1981; Amadiume, 1987).

Mwanamke kama Mrithi wa Madaraka

Kipengele kingine kinachojitokeza katika usawiri wa mwanamke wa kimfumojike ni nafasi yake kama mrithi wa madaraka na mwendelezo wa taasisi ya uongozi. Katika makala hii, dhana ya urithi haimaanishi kwamba kila mfumo wa kimfumojike lazima uwe wa urithi wa upande wa mama, bali inahusu namna matini zinavyomjenga mwanamke kama mhusika anayestahili kupokea, kumiliki na

kuendeleza mamlaka ndani ya mfumo maalumu wa kijamii. Mtazamo huu unaendana na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inayosisitiza kuchunguza mamlaka ya mwanamke kwa kuzingatia historia, utamaduni, ukoo na taasisi za jamii (Amadiume, 1997; Nnaemeka, 2004).

Katika *Mama Mtakatifu*, usawiri wa Linda Zawadi kama mrithi wa madaraka unaonekana wazi katika kauli inayomhusisha na urithi wa Mama Mtakatifu: "Ewe Linda Zawadi mtoto wa kike wa Mama Mtakatifu, kalia kiti hiki cha enzi utawale wananchi wa nchi hii ya Haki kama vile Mamako alivyotawala" (uk. 29). Dondoo hili linamjenga Linda kama mrithi anayestahili kuingia katika nafasi ya uongozi kwa kuhusishwa moja kwa moja na mtawala aliyemtangulia. Kauli "mtoto wa kike wa Mama Mtakatifu" inaunganisha mamlaka yake na ukoo wa kike, huku "kalia kiti hiki cha enzi utawale" ikionesha kwamba urithi huo unahusisha matumizi halisi ya mamlaka. Hivyo, Osodo anamjenga mwanamke kama sehemu ya mwendelezo wa taasisi ya uongozi badala ya mhusika aliye nje ya mfumo wa mamlaka.

Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, usawiri huu ni muhimu kwa sababu mamlaka ya Linda hayaelezwi kwa kumweka katika ushindani wa moja kwa moja na wanaume, bali kupitia uhusiano wake na historia na taasisi ya jamii. Hali hii inaendana na msisitizo wa Amadiume (1997) kwamba nafasi na mamlaka ya wanawake katika jamii za Kiafrika zinapaswa kuchunguzwa kwa kuzingatia mifumo mahususi ya kijamii na kiutamaduni. Kwa hiyo, urithi wa Linda unaonesha namna mwanamke anavyoweza kuwa mhifadhi na mwendelezaji wa taasisi ya uongozi.

Katika *Kivuli Kinaishi*, usawiri wa mwanamke kama mrithi wa madaraka unajitokeza kupitia Bi Kirembwe. Anajitambulisha kwa kusema: "Mimi ndiye mrithi wa jadi wa Giningi. Ndiye mchawi mkuu" (uk. 70). Anaendelea kusisitiza kuwa yeye ndiye "mwenye kustahiki kukalia kiti hiki" na anataka kukalia kiti hicho "daima dawamu" (uk. 70–71). Dondoo hizi zinaonesha kwamba mamlaka yake yanahusishwa moja kwa moja na urithi wa jadi na haki ya kushikilia kiti cha utawala. Kauli "mrithi wa jadi wa Giningi" inafafanua chanzo cha uhalali anaodai, ilhali "mwenye kustahiki kukalia kiti hiki" inaonesha namna anavyojitambua kama mwenye haki ya kumiliki mamlaka.

Kwa mujibu wa Nnaemeka (2004), nafasi ya mwanamke katika mazingira ya Kiafrika inapaswa kueleweka kwa kuzingatia mahusiano ya kijamii, historia na mifumo ya kitamaduni inayomzunguka. Kwa msingi huo, Bi Kirembwe hasawiriwi tu kama mwanamke mwenye mamlaka, bali kama mrithi wa taasisi ya jadi inayompa msingi wa kudai uongozi. Hata hivyo, kauli yake ya kutaka kukalia kiti "daima dawamu" (uk. 71) inaonesha kwamba urithi wa mamlaka unahusisha pia namna mhusika anavyotaka kuyashikilia na kuyaendeleza. Kwa hiyo, tamthilia hizi zinamsawiri mwanamke kama mrithi, mmiliki na mwendelezaji wa mamlaka ndani ya mifumo maalumu ya kijamii na kiutamaduni.

Hitimisho

Makala hii imechunguza usawiri wa mwanamke wa kimfumojike katika tamthilia za *Mama Mtakatifu* ya Felix Osodo na *Kivuli Kinaishi* ya Said Ahmed Mohamed kwa kuongozwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Uchambuzi umeonesha kuwa tamthilia hizi zinamjenga mwanamke kama mhusika mwenye nafasi katika uongozi, mamlaka ya kufanya maamuzi, ushiriki katika taasisi za jamii, ustawi wa wananchi na urithi wa madaraka. Katika *Mama Mtakatifu*, Linda Zawadi anasawiriwa kama mrithi wa uongozi anayefanya maamuzi na kuchukua hatua kuhusu mahitaji ya wananchi, huku *Kivuli Kinaishi* ikimjenga Bi Kirembwe kama mrithi wa jadi wa Giningi mwenye mamlaka makubwa ya kutawala.

Aidha, uchambuzi umeonesha kuwa mamlaka ya mwanamke hayawasilishwi kwa maana moja. Linda Zawadi anahusishwa na matumizi ya mamlaka katika kukabiliana na baadhi ya mahitaji ya jamii, ilhali Bi Kirembwe anaoneshwa katika mazingira ambamo mamlaka yake yanaweza pia kuathiri uhuru na maisha ya wanajamii. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, tofauti hizi zinaonesha umuhimu wa kumchunguza mwanamke ndani ya mazingira yake ya kijamii, kiutamaduni na kihistoria. Hivyo, tamthilia hizi zinapanua usawiri wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili kwa kumjenga kama mtendaji, mrithi na mwenye mamlaka, huku zikionesha pia wajibu unaoambatana na matumizi ya mamlaka hayo.

Marejeleo

Amadiume, I. (1987). *Male daughters, female husbands: Gender and sex in an African society*. Zed Books.

Amadiume, I. (1997). *Re-inventing Africa: Matriarchy, religion and culture*. Zed Books.

Balisidya, M. L. (1982). The image of the woman in Tanzanian oral literature: A survey. *Kiswahili, 49*(2), 1–31.

Chesaina, C. (1987). *Women in African drama: Representation and role* [Doctoral dissertation, University of Leeds].

Lihamba, A. (1979). *The image of women in the performing arts: Women's image in Tanzania literature*. BRALUP.

Mbughuni, P. (1982). The image of woman in Kiswahili prose fiction. *Kiswahili, 49*(1), 15–24.

Mohamed, S. A. (1990). *Kivuli kinaishi*. Oxford University Press.

Nnaemeka, O. (2004). *The politics of (m)othering: Womanhood, identity and representation in Africa*. Routledge.

Osodo, F. (1982). *Mama mtakatifu*. Heinemann Educational Books.

Oyěwùmí, O. (1997). *The invention of women: Making an African sense of Western gender discourses*. University of Minnesota Press.

Steady, F. C. (Ed.). (1981). *The Black woman cross-culturally*. Schenkman Publishing Company.

Strathern, M. (1987). *Dealing with inequality: Analysing gender relations in Melanesia and beyond*. Cambridge University Press.